**MWONGOZO WA USHIRIKI WA TANZANIA KATIKA MAONESHO YA DUNIA YA EXPO2020 DUBAI**
**TAREHE 01 OKTOBA, 2021 HADI 31 MACHI, 2022**

## 1.0 UTANGULIZI

Tanzania ni Miongoni mwa nchi 191 zinazoshiriki kwenye Maonesho ya Dunia ya EXPO2020 Dubai ambayo yameanza rasmi tarehe 01 Oktoba, 2021 na yanatarajia kumalizika tarehe 31 Machi, 2022. Ushiriki wa Tanzania unaratibiwa na Wizara ya Viwanda na Biashara kupitia Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade), Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda – Zanzibar, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kupitia Ubalozi wa Tanzania nchini UAE, Taasisi za Serikali na Sekta Binafsi.

Kaulimbiu Kuu ya Maonesho haya ni *“Connecting Minds, Creating the Future”*, inayolenga kuleta fikra za dunia pamoja kwa lengo la kupata ufumbuzi wa changamoto mbalimbali zinazoikabili.

Tanzania inashiriki katika eneo la ***Mobility*** yenye kauli mbiu ndogo isemayo ***“Connectivity, Tanzania Ready for Take Off”*** ambayo inaonesha utayari wa Tanzania kuwa Kitovu cha Biashara Barani Afrika kwa kuiunganisha Afrika na Dunia.

## 2.0 AINA ZA USHIRIKI

Ushiriki wa Tanzania katika Expo2020 Dubai umegawanyika katika maeneo makuu matatu (3) kama ifuatavyo: -

**2.1** Banda Kuu la Tanzania (kuanzia 01Oktoba,2021 – 31 Machi,2022);
**2.2** Programu maalum (za siku 5 – 10 kuanzia Mwezi Novemba, 2021 – Machi 2022); na
**2.3** Soko la Expo2020 Dubai kwa njia ya Mtandao (Expo2020 World Market Souq).

## 3.0 UTARATIBU WA USHIRIKI

Taratibu za ushiriki katika makundi hay ani kama ifuatavyo:-

### 3.1 Banda Kuu la Tanzania

Ushiriki katika Banda Kuu la Tanzania unahusisha Wizara, Taasisi za Serikali na Jumuiya za Wafanyabiashara (Private Sector Apex Organizations) ambazo zimebeba Kauli mbiu ya Maonesho. Utaratibu wa Ushiriki kundi hili ni kama ifuatavyo;-

i. Kuthibitisha ushiriki kwa kujibu barua ya Mwaliko kutoka TanTrade;
ii. Kuwasilisha majina ya maofisa/ wawakilishi pendekezwa na kuanisha mahitaji yao na kufanya Maombi ya Visa;na
iii. Kulipa gharama za ushiriki kiasi cha Dola za Kimarekani **2000** kwa kutumia *control number* kutoka TanTrade.

### 3.2 Programu (Siku 5 – 10) – kuanzia Watu 10

Ushiriki wa Programu unahusisha kundi la watu 5-10 na unajumuisha mtu binafsi, Taasisi au Jumuiya za Wafanyabiashara. Washiriki hao watapaswa kujaza Fomu ya maombi kwa kupakua katika Tovuti ya Mamlaka (www.tantrade.go.tz). Programu maalum zitatayarishwa kwa kushirikiana na Wadau ili kuhakikisha kuwa malengo yao yanazingatiwa.

Ili kushiriki, Kila Mshiriki atalipa kiasi **cha Dola za Kimarekani $2,221** zinajumuisha tiketi ya ndege, malazi, Mikutano 3 na usafiri wa ndani kwa siku 5 za programu. Gharama hizi zitaongezeka kadri siku zinavyoongezeka.

#### 3.2.1 Aina ya Programu

Kuna aina tatu za programu zinazoratibiwa: -

i. Programu za Kibiashara – Programu hizi ni zile zenye malengo ya kibiashara tu. Programu hizi zitakutanisha Wadau na Wanunuzi, Wabia, Watengenezaji wa teknolojia na Wawekezaji kwa lengo la kufanya biashara (Business);
ii. Programu za matembezi – Programu hizi ni kwa Wadau ambao wanakwenda Expo kutembea na kupumzika (Leisure);
iii. Programu za kujifunza – Programu hizi ni za Wadau ambao wana wanakwenda Expo kujifunza tu (Exposure and learning).

#### 3.2.2 Ushiriki wa Programu za Kibiashara, Kujifunza na Kutembea

Wadau wanaotaka kushiriki programu hii watafuata utaratibu ufuatao: -

i. Kuandika barua TanTrade ikiainisha yafuatayo –

a) Malengo ya safari

b) Idadi ya makampuni
c) Aina ya Kampuni au Taasisi ambazo wanatakiwa kukutana nazo
d) Kuwasilisha wasifu wa Kampuni au Taasisi;

ii. Kupokea barua ya uthibitisho kutoka TanTrade
iii. Kulipia gharama za ushiriki kwa kutumia *control number* kutoka TanTrade na kufanya malipo
iv. Kufanya maombi ya kupata VISA;

**3.2.3 Mambo muhimu ya kuzingatia**

i. Wasifu wa kampuni (company profiles) uandikwe kitaalam
ii. Kwa wenye kutafuta Wabia; Miradi iandikwe kitaalamu na kuwe na ripoti ya *feasibility study na environmental impact assessment*
iii. Wafanyabiashara wanatakiwa kuzingatia uwezo wa kuhudumia soko
iv. Kampuni iwe imesajiliwa na kupata Leseni ya Class A
v. Bidhaa ziwe na vyeti vya ubora na Cheti cha Uasili (certificate of origin)

3.2.4 **UUZAJI WA BIDHAA KWA NJIA YA MTANDAO (WORLD** MARKET SOUQ)

Kampuni yenye vigezo stahiki itaruhusiwa kuuza bidhaa zake kwenye Mfumo wa Soko la Mtandaoni Expo2020 Dubai (World Souq – www.expo2020dubai.com)

i. Bidhaa iwe na rajamu na jina lililosajiliwa;
ii. Bidhaa iwe na uhai usiopungua miezi 24 (24 months shelf life);
iii. Bidhaa iwe na vigezo vya Kimataifa ikiwemo vyeti vya ubora, alama ya msimbomilia (Barcode, TBS/ZBS, ISO);
iv. Bidhaa za vyakula zioneshe bidhaa zilizotumika kuitengeneza (Ingredients) na taarifa muhimu za lishe (nutritious information);
v. Bidhaa zote zioneshe ujazo au uzito (metric weight);
vi. Bidhaa zioneshe tarehe ya kuzalishwa na kumalizika (production and expiry date);
vii. Picha ya bidhaa husika (Front and back label image with High resolutions);
viii. Bidhaa za nyama ziambatishwe na cheti cha Halal;

ix. Bidhaa zote ambazo zinahitaji kibali maalum mfano Maliasili au bidhaa za Kitaifa lazima zioneshe kibali kutoka Mamlaka husika;

x. Bidhaa zote za vyakula ziwe zimethibitishwa na Mamlaka za Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) au Wakala (Food Suppliers) waliothibitishwa na Serikali ya UAE.

**NB:** Tafadhali pakua **Expo 2020 Business App** kutoka Play Store kwa watumiaji wa simu janja za Android na iStore kwa watumiaji wa simu janja za iPhone. App hii inarahisisha ufanyaji biashara kwa njia ya mtandao na inakutanisha na Washiriki wa Expo2020 Dubai kujiunga ni **$3** (hii ni gharama ya Waandaaji wa Expo2020).

### 3.2.5 **Sifa za Mwombaji**

Mwombaji anatakiwa kuwa na sifa zifuatazo: -

i. Awe na Kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria za Tanzania;
ii. Awe na Leseni hai ya kufanya biashara;
iii. Awe na vibali vinavyomruhusu kufanya biashara (madini, maliasili, uvuvi, mifugo) kutoka kwa Mamlaka husika;
iv. Awe na uwezo wa kufanya biashara za Kimataifa;
v. Awe na Namba ya Mlipa Kodi kutoka TRA;
vi. Awe amepata Chanjo ya UVIKO-19 (Sharti la Serikali ya UAE) ;
vii. Apime UVIKO-19 masaa 72 kabla ya kuondoka nchini.

## 4.0 GHARAMA ZA USHIRIKI KWA KATIKA EXPO2020 DUBAI

| **Na.** | **Tukio** | **Kiasi cha makadirio ya Gharama (US $)** |
|---|---|---|
| | **A. Banda la Tanzania** | |
| | Malipo ya gharama za ushiriki kwa kila Taasisi | 2,000 |
| | **B. Programu – kwa mtu mmoja** | |
| 1. | Ushiriki katika Mikutano ya Biashara (B2B) | 350 |
| **1.** | **Usafiri** | |
| | - **Tiketi ya ndege DSM – Dubai - DSM** | 650 |
| | - **Usafiri ndani ya Dubai** | 50 |
| **2.** | **Gharama ya Dubai Expo VISA (siku 30)** | 171 |
| **6** | **Gharama ya Malazi** | 750 |
| **7** | **Kiingilio Uwanja wa Expo2020 Dubai** | 150 |
| **8** | **Gharama ya kupima UVIKO-19** | 100 |
| | **Jumla ya gharama kwa siku tano** | **2,221** |

## 5.0 UTARATIBU WA KUPATA VISA

VISA za Expo zina utaratibu maalum na ni Visa za siku 30. TanTrade inaratibu upatikanaji wa VISA kwa utaratibu ufuatao: -

i. Mwombaji atume barua ya maombi kwa Mkurugenzi Mkuu TanTrade ya kuomba visa, iambatanishwe na majina ya wanaotaka visa.
ii. Maombi yaambatishwe na taarifa zifuatazo: -
   a) Majina kamili kama inavyoonekana kwenye pasi kusafiria;
   b) Wadhifa wa Mwombaji (designation) Job Tittle;
   c) Nambari ya Pasi ya kusafiria;
   d) Tarehe ya mwanzo na mwisho wa matumizi ya Pasi ya kusafiria (lazima ibakishe angalau miezi sita 6 kabla ya kumalizika kwa muda wake);
   e) Tarehe ya safari na muda wa kukaa Expo;na
   f) Uthibitisho wa chanjo ya UVIKO-19 na aina ya chanjo kutoka kwa Mamlaka husika.
iii. TanTrade itatuma barua iliyokidhi vigezo vyote kwa Balozi wa Tanzania Dubai ambaye ndiye Kamishna Jenerali wa Tanzania kwa ajili ya kuombewa Kibali;
iv. Baada ya Mhe. Balozi kutoa kibali; TanTrade itaingiza taarifa kwenye mfumo maalum wa Visa unaoratibiwa na Waandaaji wa Expo kwa ajili ya maombi ya VISA;
v. Serikali ya UAE kupitia Mamlaka zake itafanya uhakiki wa taarifa zilizoingizwa na TanTrade kwenye mfumo;
vi. Baada ya Uhakiki kukamilika, Serikali ya UAE itatuma VISA ya kielektroniki ka njia ya Barua pepe iliyosajiliwa wakati wa kuingiza taarifa kwa ajili ya nakala (printing).

### 5.1 Nyaraka zinazotakiwa

Zifuatazo ni nyaraka zinazotakiwa: -

i. Nakala ya pasi ya kusafiria yenye rangi;
ii. Cheti cha chanjo ya UVIKO-19;
iii. Picha ya *passport size* yenye *background* nyeupe;
iv. Nakala ya vyeti elimu (Academic certificates) if any.

**NB:** Maombi yanatakiwa kufanyika siku 14 – 30 kabla ya safari kutokana na taratibu za mfumo wa Expo kuchukua muda. Hii itapunguza changamoto wakati wa safari.
Nyaraka zote zitume kwa mfumo wa picha (JPG/JPEG)

## 6.0 UTARATIBU WA KUTUMA MAOMBI YA USHIRIKI KATIKA EXPO2020 DUBAI

Maombi yote yatumwe kwa kutumia anuani ifuatayo: -

Mkurugenzi Mkuu,
Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade),
S.L.P 5402,
**DAR ES SALAAM.**

**Barua pepe:** info@tantrade.go.tz;

### 6.1 Ushiriki wa Banda kwenye Banda la Tanzania

**Baruapepe:** getrude.ngwehemi@tantrade.go.tz
**Simu (WhatsApp):** +255 754265822

### 6.2 Ushiriki wa Programu: -

**Baruapepe:**masha.hussein@tantrade.go.tz;
magdalena.shirima@tantrade.go.tz ;
john.fwalo@tantrade.go.tz ;
cecilia.mwandepa@tantrade.go.tz ;
margaret.kiama@tantrade.go.tz

**Simu:** 0715988299; 0738397143; 0767285252; 0717478806

### 6.3 Mratibu Dawati la Expo - Wizara ya Viwanda na Biashara:

Kokuhaisa Katwire
Barua pepe: kokuhaisa.katwire@mit.go.tz **Simu**: +255685 862 325

### 6.4 Mratibu Dawati la Expo - Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda - Zanzibar;

Zawadi Zaidu Nyange

**Barua pepe:** zawadi.nyange@tradesmz.go.tz **Simu:** +255777481214

### 6.5 Masuala ya VISA

**Baruapepe:** leah.msaga@tantrade.go.tz **Simu:** 0655443871

**6.6 Usafirishaji mizigo na masuala ya forodha: -**

**Baruapepe:** thomas.mallya@tantrade.go.tz /deo.shayo@tantrade.go.tz
**Simu:** 0758001021/ 0736581010

**6.7 Mifumo ya Expo2020: -**

**Baruapepe**:loserian.laizer@tantrade.go.tz, andrew.mkangaa@tantrade.go.tz **Simu:** (WhatsApp) +255713477210/ 0788370311

**NB:** Au fika Ofisi zetu zilizopo Uwanja wa Maonesho wa Mwl. J.K. Nyerere, Barabara ya Kilwa Dar es Salaam, Ofisi za Kurugenzi ya Biashara, Mtaa wa Malindi Zanzibar, Jengo la Kilimo V, Barabara ya VETA, Dodoma.

## 7.0 UTARATIBU WA MALIPO

Malipo yote yatalipwa kwa Dola za Kimarekani au sawa kwa Shilingi za Tanzania (equivalence) na yafanyike kupitia Akaunti zifuatazo: -

### 7.1 Akaunti ya Dola za Kimarekani

| | |
|---|---|
| Jina la Akaunti: | Tanzania Trade Development Authority |
| Benki: | National Bank of Commerce |
| Namba ya Akaunti: | 012105014907 |

### 7.2 Akaunti ya Shilingi

| | |
|---|---|
| Jina la Akaunti: | Tanzania Trade Development Authority |
| Benki: | National Bank of Commerce |
| Namba ya Akaunti: | 011103026423 |

## 8.0 UTARATIBU WA KUUZA BIDHAA NDANI YA EXPO

Taasisi au Kampuni zitakazouza bidhaa ndani ya Expo2020 Dubai zitafuata taratibu zifuatazo: -

8.1 Kujaza fomu za bidhaa fomu ya *Commercial Items* na kuituma TanTrade angalia Kifungu Na. 8.0 kifungu kidogo 8.4

8.2 Waandaaji watahakiki bidhaa na kutoa kibali cha kuzisafirisha

8.3 Kabla ya kuuza mzigo unalipiwa kodi za Serikali kama ifuatavyo: -

a) **VAT – 5%**

b) **Import Duty – 5% CIF** (Bidhaa zenye kilevi, zilizoongezewa sukari za kiwandani, 50% na bidhaa za tumbaku 100%)

c) **Dubai Municipality duties – 5%** *where applicable*

8.4 Mauzo yote yatakuwa yanafuatiliwa kwa karibu na Waandaaji kulingana na bei zilizowekwa kwenye fomu ya *commercial items*

8.5 Mauzo yote yataingizwa kwenye mashine ya POS

## 9.0 MANUFAA YA USHIRIKI

9.1 Kuvutia Wabia kwa ajili ya uwekezaji na kuendeleza Sekta mbalimbali za kiuchumi;

9.2 Kutoa fursa kwa Makampuni kujitangaza na kunadi bidhaa na huduma zinazopatikana nchini ili kupata masoko endelevu;

9.3 Kutangaza vivutio vya Kitalii vilivyopo nchini; na

9.4 Kutangaza lugha ya Kiswahili, utamaduni na desturi za Watanzania;

## 10.0 MAMBO MUHIMU YA KUJUA KUHUSU NCHI YA UMOJA WA FALME ZA KIARABU

| | |
|---|---|
| **Jina la Nchi:** | Umoja wa Falme za Kiarabu - (Abu Dhabi, Dubai, Sharjah, Ajman, Umm Al-Quwain, Fujairah, Ras Al Khaimah) |
| **Mji Mkuu:** | Abu Dhabi |
| **Idadi ya watu:** | 8.1 million |
| **Eneo:** | 77,700 sq km (30,000 sq miles) |
| **Lugha Kuu:** | Kiarabu |
| **Pato la ndani (GDP):** | $421.1 bilioni |
| **Dini:** | Islam |
| **Matarajio ya kuishi:** | miaka 76 (Wanaume), miaka 78 (Wanawake) |
| **Sarafu:** | Dirham |

**Kiwango cha ubadilishaji wa fedha:**

1 AED = USD 0.27 (BOT 20/10/2021)

1 AED = TZS 628.08 (BOT 20/10/2021)

**Hali ya hewa:** Joto kali Mwezi Mei – Novemba - $32^0$C - $48^0$C

Baridi Mwezi Disemba – Machi - $24^0$C - $10^0$C